THE NON-GOVERNMENTAL ORGANIZATION
MIZIZI YA MAFANIKIO
P.O.BOX 13808 ARUSHA,
PHONE: 0627 757472 / 0765 656665, Email: miziziyamafanikio@gmail.com

## TANGAZO LA UFADHILI WA MASOMO KWA VIJANA WENYE MAHITAJI

Shirika la **Mizizi Ya Mafanikio** ni taasisi isiyokuwa ya kiserikali yenye usajiri nambari **01NGO/R/5103** na makao yake yapo Mtaa wa Longdong Kata ya Sokon 1 na imejikita katika kutoa huduma ya watoto wa mitaani, watoto yatima, wajane, na mabinti wenye umri wa kwenda shule ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwasomesha ili kuwawezesha mabinti hao kufikia ndoto zao. Kila mwaka shirika linapokea maombi ya wasichana na vijana wanaopenda kuendeleza ujuzi wao.

Tunapenda kuwataarifu kuwa kwa mwaka 2025, Shirika la Mizizi ya Mafanikio linazo nafasi 25 za ufadhili wa masomo kwa vijana wanaotoka katika familia zenye hali duni kiuchumi. Ufadhili huu unalenga kusaidia vijana wenye vipaji, wanaojitahidi kielimu, lakini wanakosa fursa ya kuendeleza masomo yao kutokana na changamoto za kifedha. Nafasi 10 ni za bweni na 15 ni za kutwa.

**Sifa za Waombaji:**

1. Awe mwanafunzi kutoka familia yenye kipato cha chini.
2. Awe ameonyesha matokeo mazuri ya kitaaluma
3. Barua ya kuthibitisha hali ya kifamilia kutoka kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa.
4. Umri wa mwanafunzi uwe kati ya miaka 14 na kuendelea.
5. Awe na elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea au aliyekatisha masomo yake kwa changamoto ya kiuchumi.
6. Awe na nia ya kujifunza na kuendeleza ujuzi wake.

**Jinsi ya Kuomba:**
1. Jaza fomu ya maombi inayopatikana kwenye ofisi zetu zilizopo **sokon 1, shinda**
2. Ambatanisha nakala ya vyeti vya kitaaluma, kitambulisho cha mzazi/mlezi, na barua ya maombi ya ufadhili ukieleza kwanini upewe ufadhili.

3. Tuma maombi **kabla ya tarehe 15 /7/ 2025**. Ili kuruhusu mchakato wa nuhakiki kwa wakati aweze kuanza masomo
4. taarifa zote utakazotoa ziwe za kweli kwani kuna kutembelewa majumbani kuhakiki taarifa zako.

**Faida za Ufadhili:**

1. Ada ya shule kulipiwa kwa mwaka mzima.
2. Gharama za vifaa vya shule (vitabu, sare, nk atalipia mzazi/mlezi.
3. Kwa mwachuo wa bweni, watalipiwa Ada,malazi na chakula.

**Kozi Zinazofadhiliwa Na Shirika Ni  Pamoja Na:**

1. Kozi ya Kwanza – TEKNOLOGIA YA HABARI NA MAWASILIANO (ICT COURSE)
2. Kozi ya Pili – KOZI YA UKARANI (FULL SECRETARIAL COURSE)
3. Kozi ya Tatu- UTALII (TOUR GUIDE AND OPERATION)
4. Kozi ya Nne- HOTELIA (HOTEL MANAGEMENT)
5. Kozi ya Tano- USUSI NA UREMBO (HAIR DRESSING AND BEUTY)
6. Kozi ya Sita- UFUNGAJI UMEME WA MAJUMBANI (ELECTRICAL INSTALLATION)
7. Kozi ya Saba- UFUNDI CHEREHANI (TAILORING AND SUIT MAKING)
8. Kozi ya Nane- USIMAMIAJI WA BIASHARA (BUSINESS ADMINISTRATION)
9. Kozi ya Tisa- MAUZO NA MASOKO (SELLS AND MARKETING)
10. Kozi ya Tisa -WA UALIMU WA AWALI (ECED)
11. Kozi ya Tisa -WA MASOMO YA KILIMO NA MIFUGO (Animal Husbandry  12. Kozi ya Tisa - UFUNDI BOMBA (plumbing)

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia:

Simu: 0765656665/0627757472
Barua pepe: **miziziyamafanikio@gmail.com**

Imetolewa na

Mkurugenzi Mtendaji

**SHIRIKA LA MIZIZI YA MAFANIKIO.**